**Noa Bongo ! Jenga Maisha Yako !**

**Utandawazi : Kandarasi za Kilimo Cameroon**

**O-Töne : Henri Fotso**
**Text : Sandrine Blanchard**
**Redaktion : Yann Durand**
**Übersetzung : Anne Thomas**

---

**3 Stimmen …………Sauti 3 :**

- **junger Sprecher 1 ……………..Msimulizi wa kiume 1**
- **junger Sprecherin 1 ………….. Msimulizi wa kike 1**
- **Sprecher(in) 2…………………Msimulizi wa kike 2 als Off-Stimme für die Reportage**

---

**Vorspann LbE……………………………..Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA - REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :**

Habari gani ! Natumai nyote hamjambo !

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Leo katika mfululizo wetu kuhusu utandawazi tutazungumzia juu ya kilimo cha kandarasi au kwa maneno mengine cha mikataba.

**Msimulizi wa kike 1 :**

Kuhusu wakulima ambao husaini mikataba na makampuni makubwa ya kimataifa.

**1.Atmo Land + Auto unterlegen………………**

**- 2 -**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Na tutakuwa tunaelekea huko Limbe na Tiko vijiji viwili vilioko kusini magharibi mwa Douala mji mkuu wa Cameroon.

**Msimulizi was kike 1 :**

Vijiji viwili ambapo kilimo cha kondarasi ni jambo la kawaida tu..

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Msimulizi wa kike 1 + Msimulizi wa kiume 1 :**

Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari !

**……………………..Manuscript ………………………………..**

**1.Atmo hoch dann unterlegen………….**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Mlima Cameroon una urefu wa mita 4,090 na unaangalia Bahari ya Atlantiki.Kuna mashamba ya ndizi,mawese na mipira…. hapa Tiko mashamba hayo yamekuwa yakiendelea kuwepo na kuendelea kuwepo hadi milele.Mengi ya mashamba hayo yalioko chini ya mlima yanaendeshwa na Shirika la Maendeleo la Cameroon au CDC.

**1.Atmo hoch dann ausblenden……………..**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Mayah Godfred Che anatupokea katika ofisi yake huko Limbe yeye ni mtaalamu wa takwimu katika shirika la CDC.

**- 3 -**

**2.CDC 1 (anglais) fängt mit Türgeräusch an …….**

Kwa kadri shirika la CDC linavyohusika tuna mashamba saba ya mafuta ya mawese tuna mitambo miwili ya mafuta na tuna jumla ya hekta 11,729 ya eneo ambalo tayari limekwisha tayarishwa na ambako ndiko tunakowekeza hivi sasa.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Kilimo kinazidi kuwa kikubwa sana kila uchao.Na sura ya kijiji cha iko inaanza kubadilika.

**3.Atmo Fällen ……………………..**

**4.CDC 3 (anglais)**

Watu wenye kupanda mashamba yao wenyewe huwa wanapanda na kuvuna mazao na hutuleteya sisi kuyanunuwa na huwa tunayanunuwa kwa idadi na kwa tani.Wakulima hao ni muhimu kwa sababu wanasaidia kuongeza kima cha uzalishaji wetu.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Kokwa za michikichi zinazovunwa na wakulima wadogo huvunjwa na kiwanda cha mafuta cha shirika la CDC na baadae shirika hilo husafirisha mafuta yake ya mawese duniani kote.

**Atmo Fabrik …………………….**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Wakulima hupata fungu la faida kwa mfano kwa kupatiwa mashine za kilimo.Hata hivyo kwa upande wa pili wa sarafu wakulima wao huwa wanaitegemea mno kampuni hiyo.Hebu na tusikilize kile anachofikiria Gabriel Mbene ambaye ni rais wa

chama cha wakulima wa kienyeji na makamo wa rais wa Chama cha Vyama Huru vya Wafanyakazi cha Cameroon.

**6. Gewerkschaft (English)**

Kwa kweli wadau hawa wadogo,wanaopanda mazao ambao huitwa wakulima wadogo wenye kutegemea uzalisha mdogo sana wa mazao wa kama hekta moja au mbili kwa hakika sio rahisi kuwa na soko la kuuzia mazao yao na soko lao pekee kwa hivi sasa linapaswa tu kuwa makampuni haya makubwa ya kilimo kama vile CDC.

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Kwa hiyo kimsingi kuna uwiano usio sawa wa madaraka kati ya kampuni na wakulima wadogo ?

**Msimulizi wa kike 2 :**

Tunaweza kusema siku nyengine uhusiano huo unakwenda kombo kidogo …..tusikilize maelezo ya Thomas.

**7.Atmo Nüsse**

**+8.Thomas Vorstellung**

Jina langu ni Nughewe Thomas.Nilikuwa nikipanda michikichi kwenye shamba kwa ajili ya mafuta ya mawese lakini kampuni ya CDC ilituzuwiya.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Thomas alitupokea kwenye uwa wake huko Tiko.Haendi tena shambani pamoja na wanakijiji wenzake wengine ….tokea kuzuka kwa matatizo yake na CDC ambayo ilimfilisi.

**8.wieder Atmo Nüsse**

**Msimulizi wa kike 2 :** Hapo mwanzoni kila kitu kilikuwa sawa.Kama ilivyo kwa wakulima wengine katika eneo hilo mkulima huyo alisaini mkataba na kampuni ya CDC ambapo alikubali kuuza kokwa zake zote za michikichi kwa kampuni hiyo na CDC iliahidi badala yake kununuwa mazao yake na kumpatia zana mpya za kilimo.

**9.Thomas Zahlung**

Tatizo ni kwamba wakati ninapowapatia mazao hushindwa kunilipa.Hapo tena huwa nashindwa kuwalipa watu wanaofanya kazi shambani.Lakini watu hao huwa wanataka kulipwa wakati wanapoondoka shambani hapo jioni ….wananitaka nihesabu kile walichokikata na niwalipe fedha zao.

Imeichukuwa kampuni ya CDC miezi mitatu kumlipa Thomas fedha hizo.Ilibidi achukuwe mkopo ili kuweza kuwalipa wafanyakazi wake 10.Baadae mkulima huyo akaamuwa kuuza kokwa zake za mchikichi kwa kampuni ya Socapalm ambayo ni mshindani mkubwa wa kampuni ya CDC.Kampuni ya CDC ikaiona hatua ya mkulima huyo kuwa ni usaliti na ikataifisha zana iliokuwa imempa aitumie wa shughuli zake za kilimo. Thomas anadai kwamba CDC iliwahi kuwaajiri majambazi kuiba mavuno yake wakati wa usiku.Amesema kwamba kampuni hiyo ilikuwa ikimpelekea vitisho.Hata hivyo kaka yake naye ambaye alikuwa mshirika wake aliacha biasahara hiyo ya kilimo.

**Msimulizi wa kiume 1 (whispers ….akinon’gona)**

Lakini Thomas na wafanyakazi wake wa zamani wanafanaya nini hivi sasa ?

**Msimulizi wa kike 1 (whispers …….akinon’gona)**

Naam baadhi yao wanafanya kazi na waajiri wengine lakini wengi wao wanaishi katika shida.

**10.Thomas Schulden**

Leo maisha yamekuwa magumu hatuna ajira.Wanawake wengine wanaanguwa kilio na kuuliza watoto wataishi vipi ? Nashindwa hata kulipa kodi na nina malimbikizo yake ya miaka mingi …. siwezi kulipa kodi hiyo.

**Msimulizi wa kike 2 :** Yumkini ikamuia vigumu kwa Thomas kupata kazi tena.Lakini vyama vya wafanyakazi wakulima vimekuwa vikidai makampuni makubwa yenye kuendesha mashamba ya eneo hilo pia yawawezeshe wakulima na wanakijiji wafaidike mfano kwa kuwajengea barabara au kuwapatia ruzuku ili kwamba waweze kununuwa mbolea na kuwalipa wafanyakazi.

**Musik hoch dann unterlegen und ausblenden………**

---

**SEHEMU YA PILI   ERKLÄRSTÜCK**

**Msimulizi wa kike 1 na Msimulizi wa kiume 1 tu !**

**Msimulizi wa kiume :** Iwapo nimefahamu vyema kilimo cha kondarasi kinawaunganisha wakulima na shughuli za viwanda vya kilimo cha chakula.

**Msimulizi wa kike :** Hasa! Kampuni kubwa huwa zinafanya makubaliano na wakulima na kukubaliana kununuwa mazao yao yote.Kwa njia hiyo kampuni huwa zinaweza kujuwa kwamba zitakuwa na mali ghafi za kutosha.

**Msimulizi wa kiume :** Na je kilimo cha kondarasi kiko barani Afrika tu ?

**Msimulizi wa kike :** Hapana ! Kilianzia nchini Marekani katika miaka ya 1950. Baadae kikaingia Ulaya ambapo kiliendelea na

shughuli za viwanda vya vyakula.Kilimo cha mikataba pia kiko barani Asia.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini inakuwa vipi wakulima wadogo wa kujitegemea ambao kwa mfano wana biashara ya kifamilia wanakuja hasa kusaini kondarasi na makampuni makubwa ya kimataifa ?

**Msimulizi wa kike :** Kwa mfano kuna mipango mingi ya misaada inayoendeshwa na mashirika yasio ya kiserikali NGOs au na FAO.

**Msimlizi wa kiume :** FAO ?

**Msimulizi wa kike :** Hilo ni shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula. FAO ina huduma inayotowa inayoitwa Idara ya Mfumo ya Msaada wa kilimo ambayo husaidia wakulima kuboresha miundo mbinu na mbinu za uzalishaji na kuwawezesha kuyafikia masoko ya kimataifa ili kwamba waweze kuuza mazao yao.

**Msimulizi wa kiume :** Je wakulima wanaweza kulazimishwa kulima mazao ya aina moja?

**Msimulizi wa kike :** Uko ukulima wa aina hiyo wa zao moja tu.Ina maana kwamba hapo wakulima hulazimika kuachana na ukulima wao wa kuzalisha mazao ya chakula kwa kusudio la jamii ya kienyeji au kwa ajili ya familia.

**Msimulizi wa kiume :** Kuna utaratibu wa kilimo ambao huwawezesha wakulima wachanganye kilimo cha mazao ya chakula na kile kwa ajili ya mazao ya viwanda ?

**Msimulizi wa kike :** Inaonekana ni vigumu kutokana na mifumo yake kuwa tafauti …. lakini ni kweli lingelikuwa jambo la kufaa.

**Msimulizi wa kiume :**………kwa hiyo wakulima wanaweza kuwa na chakula cha kutosha na kuboresha mazingira ya utendaji wao wa kazi kwa kuzifanya kuwa za kisasa mbinu za uzalishaji …….

**Msimulizi wa kike :**…………kwa kadri watakapokuwa wanayazingatia mazingira ili kwamba ardhi na rasilmali ya asili haitumiwi yote kufikia hatua ya kumalizika.

**Abspann …………………………..Funga Kipindi.**

**Msimulizi wa kike :**

Na kufikia hapo ndio tumefikia tamati ya kipindi hiki cha Noa Bongo! Jenga Maisha Yako ! Asante kuwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi na kilimo cha kondarasi au mikataba. Ni kipindi cha Deutsche Welle klichotayarishwa na Henri Fotso na Sandrine Blanchard.Kujuwa zaidi au ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye mtandao wetu :www.dw-world/lbe: Usikose kujiunga nasi tena mara nyengine!
Kwaheri!